

**ZIARA YA MKUU WA MKOA DKT. PHILEMON SENGATI WILAYANI
KALIUA30.09.2020**

Mnamo tarehe 30/09/2020 Mkuu wa mkoa wa Tabora Dkt Philemon Sengati alifanya ziara katika halmashauri ya wilaya ya Kaliua na alikuja kwa masuala makuu mawili ambayo ni uzinduzi wa eneo la ujenzi wa kituo cha afya cha kata ya Usinge na pili kwa ajili ya masuala ya TASAF.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Kaliua Ndg. Jerry Mwaga alipokuwa akimkaribisha Mkuu wa mkoa Dkt Philemon Sengati azungumze na wananchi wa kata ya Usinge, alimweleza Mkuu wa mkoa pamoja na wananchi mchanganuo wa fedha zilizotolewa katika kituo hicho cha afya, pia aliishukuru kampuni ya JTI kwa kuahidi kutupatia shilingi milioni mia tano (500,000,000) kwa ajili ya majengo mengine ya kituo hicho cha afya



Kwa upande wake Mkuu wa wilaya Mhe. Abel Yeji Busalama alimshukuru Mkuu wa mkoa wa Tabora Dkt Philemon Sengati kwa kuja kutuunga mkono katika kuanza kwa ujenzi wa kituo na kusaidia Kampuni ya JTI kutuletea fedha zitakazotumika kujenga majengo ya kituo hicho.



Baada ya hapo Mkuu wa mkoa wa Tabora Dkt Philemon Sengati aliongea na wananchi katika eneo lililoandaliwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha kata hiyo, Mkuu wa mkoa aliwaeleza wananchi jinsi Serikali ya awamu ya tano ilivyodhamiria kusogeza huduma mbalimbali karibu na wananchi kama vituo vya afya kila kata na zahanati kila kijiji na pia kusambazwa kwa umeme na maji katika kila kijiji.

Pia aliwataka wahandisi kusimamia ujenzi wa majengo yote kwa umakini ili ubora wa jengo uendane na thamani ya fedha iliyotolewa.



Mkuu wa mkoa Dkt. Philemon. Sengati akizungumza na wananchi wa kata ya Usinge



Baada ya hapo Mkuu wa Mkoa wa Tabora alishiriki pamoja na wananchi wa Usinge kuchimba msingi wa jengo la maabara katika eneo hilo la kituo cha afya kuashiria kuanza kwa kazi ya ujenzi wa majengo ya kituo cha afya cha kata ya Usinge.



Pia viongozi mbalimbali walishiriki katika zoezi hilo la uchimbaji wa msingi wa maabara akiwemo Mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya Kaliua Ndg. Jerry Mwaga, Mkuu wa wilaya wa Kaliua Pamoja na Katibu Tawala wa wilaya ya Kaliua.



Wananchi na viongozi mbalimbali wakichimba msingi wa jengo la maabara katika kituo cha afya katika kata ya Usinge

Baada ya uchimbaji wa msingi huo, Mkuu wa mkoa alielekea kata ya Igagala ambapo alifanyikiwa kufika nyumbani kwa walengwa wa TASAF ambao alizungumza nao na wakaelezea mafanikio waliyoyapata baada ya kuja kwa TASAF kama kujenga nyumba, kununua mbuzi pamoja na kusomesha watoto wao pia walieleza kuwa maisha kabla ya TASAF yalikuwa magumu saana, waliishukuru serikali ya awamu ya tano ya Rais Dkt John Pombe Magufuli kwa kuwajali watu wenye maisha magumu na kuwasaidia.



Baada ya kumaliza kuzungumza nao, Mkuu wa mkoa alielekea eneo la mkutano katika kata ya igagala ambapo alizungumza na walengwa wote wa TASAF na kusikiliza mafanikio waliyoyapata kupitia fedha hizo, pia alisikiliza changamoto kutoka kwa walengwa kama kupewa hela zilizokatika, na wengine kutopata pesa wakati huu, Mkuu wa Mkoa aliwapatia majibu yaliyojitosheleza akishirikisha uongozi wa TASAF. kisha akaelekea kata ya Kaliua magharibi kwenye mkutano mwingine wa walengwa wa TASAF.



Mkuu wa mkoa alifika kata ya Kaliua katika kijiji cha Kaliua magharibi, Mkuu wa mkoa Dkt. Philemon Sengati akaweza kuzungumza na walengwa wa TASAF baada ya hapo aliwapongeza viongozi wote wa TASAF kwa kazi nzuri wanayoifanya pia akawashauri na kuwasisitizia walengwa wa TASAF kuwa lengo la fedha za TASAF ni kuwawezesha kuinuka kiuchumi kutoka hali duni kwenda hali ya unafuu wa maisha hivyo watu wasiende kuzinywea pombe fedha hizo.

Pia aliwonya watumishi wa afya wanaowanyima dawa wagonjwa na kuwataka wakanunue dawa hizo kwenye maduka waliyoyafungua.



Mwisho Mkuu wa Mkoa aliwahasaa wananchi kutowasilikiza wanasiasa wanawopotosha watu na kuendelea kumuunga Rais wetu mkono.